

64-0402 Yehova-Yire #1

Jaribio la Msingi

Jina: _____ Hadi: Jumapili, Desemba
31, 2023

1. Yohana alikwenda nyikani, ambako alijifunza mambo ya Mungu, akiwa na umri wa miaka _____, akatoka akiwa na umri wa miaka _____, akahubiri kwa miezi _____, Kisha akauawa.

Tisa / Thelathini / Sita

Tisa / Thelathini na tatu / Nane

Kumi na mbili / Ishirini na nane / Tatu

Saba / Ishirini / Sita

2. "Ibrahimu akapaita mahali hapo _____: kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa Bwana itapatikana."

Yehova-Yire

Yehova-rafa

Yehova-shalom

Yehova-Manase

3. Mwanadamu humtafuta Mungu. Kamwe Mungu hamtafuti mwanadamu.

Kweli

Uongo

4. Katika Warumi mlango wa 4, Je, Ibrahimu alisita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini?

Ndiyo

Hapana

5. Mungu anakutaka uamini mambo mengine ya kuchekesha sana, bali Yeye daima huyafanya kuwa ya kweli.

Kweli

Uongo

6. Shirika kubwa la kwanza ulimwenguni lilikuwa ni lipi?

Rumi

Uchina

Babeli

Yerusalemu

7. "Sasa tunaona, waliposhuka kwenda Misri, walipoteza _____ zao, lakini si _____ lao. _____ lilikuwa lingali lipo."

Matendo / Imani

Agano / Baraka

Imani / Matendo

Baraka / Agano

8. Ni Wakati gani Bwana alipomtokea Ibrahimu tena?

Hatimaye wakati alipomtii Mungu kwa utimilifu kabisa

Wakati Ibrahimu alipokuwa karibu kumtoa Isaka

Wakati Ibrahimu alipotahiriwa

Wakati Ibrahimu aliposhuka kwenda Misri

9. Kila ahadi ya Kiungu katika Neno ni mali ya Ibrahimu na Uzao wake, nawe ni mrithi wake.

Kweli Uongo

10 " _____ nanyi mta _____, kwa maana mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio."

Ombeni / Pokea

Aminini / Ona

Tafuteni / Pata

Bisheni / Funguliwa

11. Wakati Unapo _____, utaingia katika shida.

Kuwa na Wakati wa Ukimya

Sikiliza Kanda

Jitenga na waaminio

Soma Biblia yako na kuomba

12. Baada ya vita kwisha, Ibrahimu alikutana na nani aliyempa ushirika?

Sara

Lutu

Melkizedeki

Abimeleki

13. "Mungu kamwe hafanyi jambo lolote bila kwanza kuwapa watu ishara na onyo. Na ishara halisi hufuatwa na sauti, na sauti hiyo siku zote ni sauti ya_____."

Kimaandiko

Nguvu

Juu

Utulivu

14. "Mungu alimwumba mwanamume na kumvalisha kama mwanamume, na mwanamke kama mwanamke. Yeye daima anawadumisha wawe hivyo. Amina. Unapowaona wakifanya jambo tofauti, kuna kasoro fulani. Jambo hilo _____."

Linakubalika

Limepotoshwa

Ni la kawaida

Ni La kisasa

15. Ni katika wakati gani wa kanisa ambapo Neno, ambalo lilikuwa ni Kristo, lilitolewa nje, akibisha mlango, akijaribu kupata ushirikiano kutoka mahali fulani apate kuingia na kujitambulisha?

Wakati wa Laodikia

Wakati wa Filadelfia

Wakati wa Sardi

Wakati wa Efeso

16. Ni kadi gani ya maombi ambayo ndugu Branham aliita ya kwanza?

A 15

C80

B 75

Hakuita kadi yoyote

17. "Yeye daima ni _____ anayetambua mawazo na makusudi ya moyo. Kwa sababu, ni wangapi wanaojua Biblia ilisema ya kwamba, 'Neno la Mungu linatambua mawazo yaliyo ndani ya moyo'?"

Mtu wa kawaida

Mtu mtakatifu

Mtakatifu mwenye haki

Nabii

18. "Kama vile umeme utokavyo _____ hadi _____, ndivyo itakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu."

Magharibi / Mashariki

Mashariki / Magharibi

Kaskazini / Kusini

Kusini / Kaskazini

19. Ni nani ambaye alikuwa amepata funuo kwa wingi sana hata alishikwa na wasiwasi, "Naye alikuwa na shida katika mwili wake, asije akajivuna kwa wingi wa hizo funuo."?

Yohana

Paulo

Musa

Petro

20. Yule maskini mwanamke aliyekuwa amelala pale kwenye machela alifanya nini baada ya Ndugu Branham kumwita?

Aliketi pale kwa sababu hakuamini

Hakusikiliza naye akapoteza uponyaji wake

Alisimama apate kuchukua ahadi yake katika Mungu

Alikimbia kote jukwaani akimpa Mungu utukufu